



Ofisi ya Taifa ya Takwimu

Simu: +255 26 - 2963822
 Nukushi: +255 26 - 296382
 Barua pepe: sg@nbs.go.tz
 Tovuti: www.nbs.go.tz

Barabara ya Jakaya Kikwete
 S. L. P. 2683
Dodoma
TANZANIA



Kumb. Na. BE. 424/448/01/72

Tarehe: 06 Aprili, 2023

TAARIFA KWA UMMA KUHUSU WATALII WALIOINGIA NCHINI, KIPINDI CHA JANUARI - FEBRUARI, 2023

Taarifa ya mwenendo wa idadi ya watalii walioingia nchini ni mionganoni mwa taarifa za mara kwa mara (high-frequency data) zinazotolewa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu kwa mujibu wa **Sheria ya Takwimu SURA 351**. Kiashiria hiki pamoja na viashiria vingine hutumika kutathmini mwenendo wa ukuaji wa uchumi wa nchi katika vipindi vifupi.

Idadi ya Watalii Walioingia Nchini, Kipindi cha Januari - Februari 2023

Katika kipindi cha Januari - Februari 2023, idadi ya watalii walioingia nchini **waliongezeka hadi 290,896** ikilinganishwa na watalii **195,483** walioingia nchini kipindi kama hicho mwaka 2022, ikiwa ni ongezeko la watalii **95,413** sawa na asilimia **48.8**. Idadi ya watalii walioingia nchini kupitia Zanzibar walikuwa **114,169** sawa na asilimia **39.2** ya watalii wote walioingia nchini katika kipindi hicho.

Kasi ya watalii kuingia nchini imeendelea kuongezeka kutokana na nchi nyingi kuondoa zuio la wananchi kusafiri nje ya nchi baada ya kipindi cha UVIKO-19 na hatua endelevu za Serikali za kutangaza vivutio vya utalii ndani na nje ya nchi ikiwa ni pamoja na filamu ya *Tanzania, the Royal Tour*. Watalii wanaoingia nchini kwa lengo la kupumzika, kufanya biashara na kusalimia ndugu na marafiki wameendelea kuongezeka.

Idadi ya watalii walioingia nchini kipindi cha Januari – Februari 2023 walitoka katika nchi mbalimbali. Nchi sita zilizoongoza kwa kuleta idadi kubwa ya watalii walioingia nchini kutoka nchi za nje ya Bara la Afrika zilikuwa ni Ufaransa iliongoza kwa watalii 25,837 ikifuatiwa na Italia (watalii 18,556), Marekani (watalii 16,567), Ujeruman (watalii 15,705), Poland (watalii 12,369) na Uingereza (watalii 10,657). Aidha, idadi ya watalii walioingia nchini kutoka katika nchi za Bara la Afrika walikuwa kama ifuatavyo: Kenya (watalii 29,615), Burundi (watalii 16,832), Rwanda (watalii 7,627), Malawi (watalii 6,563) Uganda (watalii 6,511) na Afrika Kusini (watalii 5,196). Nchi 15 kati ya 212 ziliingiza idadi kubwa ya **watalii 189,005** sawa na **asilimia 65.0** ya watalii wote.

Idadi ya watalii walioingia nchini katika kipindi hicho mwaka 2023 walifika kwa malengo mbalimbali ikiwa ni pamoja na: mapumziko, watalii 263,934 sawa na asilimia 90.7; kutembelea ndugu na marafiki, watalii 16,307 sawa na asilimia 5.6; kuelekea nchi nyingine, watalii 6,035 sawa na asilimia 2.1; shughuli za kibiashara, watalii 3,418 sawa na asilimia 1.2; na sababu nyingine, watalii 1,202 sawa na asilimia 0.4.

*Kwa taarifa zaidi wasiliana na Mtakwimu Mkuu wa Serikali S.L.P 2683 Dodoma,
 Simu +255 26 2963822, Nukushi +255 26 296382, Baruapepe: sg@nbs.go.tz, tovuti: www.nbs.go.tz*

